



## Maswali na Majibu kuhusu historia ya ukimwi

Q. Ukimwi umetoka wapi?

Mwanzo wa ukimwi bado haujagunduliwa lakini kuna utafiti kadhaa kuhusu virusi hivi. Lakini ile inajulikana sana ni yakwamba virusi vya ukimwi vimetokana na binadamu kuhusiana na nugu, kuna virusi ambayo imnapatikana kwa nugu inayoitwa SIV ambayo inafanana na virusi vya ukimwi na inaweza kupitishwa kwa binadamu. Ugonjwa za wanyama kushika binadamu si jambo la kushangaza kwani kuna magonjwa kama Ebola, homo ya ndege. Virusi vya SIV vinafanana na virusi vya ukimwi lakini vile virusi hivi hufanya kazi na kuingia mwilini bado haijulikani kuna mifano kama kukata nyama ya nugu na kujikata na damu hizi mbili kushikana na kwa hivyo virusi kuingia binadamu.

Q. Nimesikia kuna njia zingine!

Ndio, kuna kitabu ambacho kimeandikwa na kinasema yakwamba virusi vya ukimwi vilipitishwa kwa binadamu kwa njia ya kuchanga polio nchini Congo. Lakini utafiti hadi wa leo haukubali fikra hii. Pia watu wanaamini yakwamba virusi vya ukimwi vimetengenezwa na mtu ii kuua watu, wengine husema ya kwamba viumbe ambavyo si vya hii dunia ndio wametengeneza virusi, Ingawa watu wengi wanafikiria njia hizi utafiti ambao umefanywa haukubali. Mpaka wa leo mwanzo wa ukimwi haujulikani.

Q. Inajalisha?

Ndio inajalisha, lakini hivi sasa kuna vitu za maana duniani kuliko ugonjwa wa ukimwi. Haijalishi kama virusi hivi vimetokana na nugu au vimetoka dunia nyingine. Watu milioni arubaini wana virusi hivi duniani na milioni ishirini na tano tayari wameegadunia. Cha muhimu ni kujikinga kutokana ana virusi hivi, matibabau na kuchunga wale tayari wana virusi hivi. Tukijua pale virusi vya ukimwi vimetoka hii haitabadilisha ya kwamba kuna watu ambao wana ishi na virusi hivi.

Q. Historia ya virusi vya ukimwi ni nini?

Ukimwi ulipimwa kwanza mwaka wa elfu moja mia tisa na themanini huko marekani, kutokana na damu ambazo zimewekwa virusi vya ukimwi vilikuwa hata mwaka elfu moja mia tisa hamsini na tisa. Kesi zingine zinaonesha virusi kupatikana Uganda, America, Haiti, na Tanzania miaka ya elfu moja mia isa na sabini. Utafiti unaonesha virusi hivi vilianza kudhuru binadamu miaka ya elfu moja mia tisa na thelathini na miaka ya elfu moja mia tisa na arubaini. mwaka wa elfu moja mia tisa na themanini na tatu watafiti wawili walijua ugonjwa wa ukimwi huletwa na virusi vya HIV.